NO MORE
DOMESTIC VIOLENCE

Ukatili wa majumbani

Taarifa, usaidizi na huduma katika Islington

Kama unafanyiwa vitendo vya ukatili wa majumbani, usiteseke kimya kimya

Kwa taarifa, ushauri, usaidizi au makazi ya dharura piga:

Masaa 24 Simu ya Kitaifa ya msaada Ukatili majumbani: Simu ya bure
0808 2000 247

Tumia mwongozo huu kwa usalama – fikiria ni wapi utaweka kijitabu hiki, kama mtu mwingine atakuwekea, na namna ya kujilinda wakati unasoma.

Kukiwa na dharura siku zote piga 999

Je unamwogopa mtu unayemfahamu au unayeishi naye?

Labda umetendewa vibaya na patna wako mara moja tu, au umeishi na kutendewa vibaya kwa miaka mingi. Huenda mtu unayeishi naye karibu, unafanya naye kazi au kumfahamu anafanyiwa vitendo vya ukatili.

Mwongozo huu unatoa taarifa juu ya masuala ambayo huenda yanakuhusu.

Wengi wa waliosalimika ni wanawake, lakini mwongozo huu utakuwa na manufaa kwa vyovyote uwe ni mwanamke au mwanaume uliyefanyiwa ukatili majumbani. Kila mtu ana haki sawa chini ya sheria.

Mienendo mingi inayoambatana na ukatili wa majumbani ni uhalifu na mkosaji anaweza akashtakiwa kwa makosa ya jinai na kufungwa jela.

Lakini ukatili wa nyumbani sio vitendo vya kutumia nguvu tu.Hujitokeza kwa njia nyingi tofauti lakini siku zote hukuacha ukiishi katika hofu.

Unaweza kupata taarifa zaidi na msaada kutoka kwenye shirika lolote lililoorodheshwa kwenye mwongozo huu na kwenye ukurasa wa mbele. Au unaweza kupata taarifa za kina zaidi kutoka kwenye tovuti ya Halmashauri ya Islington-

www.islington.gov.uk/domesticviolence

Kwa ushauri na taarifa piga:

Misaada kwa wanawake ya Solace:
020 8269 2121

Usaidizi wa Waathiriwa Islington:
020 7700 6014

Kikundi cha Wanawake Wanaozungumza Kituruki IMECE:
020 7354 1359

Misaada kwa Wanawake wa Kilatino wa Kiamerika:
020 7275 0321

Polisi ya Islington Kitengo cha Usalama:
020 7421 0385

Simu ya Ushauri na Maulizo ya wanaume (WANAUME):
0808 801 0327

Upinde wa mvua Uliovunjika (kwa wasagaji, wasenge, wenye jinsi mbili na waliobadilisha jinsia waliosalimika):
0845 260 4460

Wakati wa dharura piga:
999

Kwa mwongozo wa kina zaidi na kuangalia huduma za karibu na za kitaifa nenda kwenye:

www.islington.gov.uk/domesticviolence

sip Safer Islington Partnership
METROPOLITAN POLICE Working together for a safer London
LFB LONDON FIRE BRIGADE making London a safer city
Islington NHS Primary Care Trust
ISLINGTON

Kumbuka: Huko peke yako. Msaada unapatikana.

Ukatili wa majumbani

Unyanyasaji wa kijinsia
Kubaka, simu za maneno machafu, kuingiliwa kwa nguvu kwa njia ya kuma au mkundu,kulazimishwa kutazama au kutenda vitendo vya kiponografia, kusemeshwa kwa njia ya kudhalilishwa nk.

Unyanyasaji wa kifedha
Kuwekwa bila fedha, kulazimishwa kutoa maelezo ya matumizi, kulazimishwa kulipa bili, kulazimishwa kutoa fedha yote ya mshahara, ruzuku au malipo ya pensheni.

Bughudha
Kuchungwa, kuandamwa, kusumbuliwa, Kutumiwa simu/barua zisizohitajika, kutishwa nk.

Unyanyasaji wa kimwili
Kupiga, kupiga ngumi, kupiga kofi, kuuma meno, kuunguza, kupiga teke n.k.

Unyanyasaji wa kihisia
Kutukanwa kwa maneno na kuaibishwa, kudhalilishwa mbele za watu, kutengwa na familia na marafiki, kebehi za mara kwa mara au ukosoaji n.k.

1 Komesha ukimya

Unayo haki ya kuishi maisha yasiyokuwa na ukatili wala hofu. Kumbuka.....

- **Huko peke yako:** Utafiti unaonyesha kuwa katika kila wanawake kumi kuna mmoja ambaye yuko kwenye uhusiano wa kinyanyasaji. Inatokea kwa wanawake wenye umri zote, matabaka, makabila na dini.
- **Huna lawama:** Patna wako/mkosaji anayo hiari ya kuchagua mwenendo atakaofuata.
- **Huwezi kubadilisha mwenendo wa patna wako:** Njia pekee ya mkosaji kubadilika ni yeye kutambua kuwa ana tatizo na kuomba msaada.
- **Uko hatarini kama utapuuzia ukatili:** Ukatili hua unaongezeka kadri muda unavyopita
- **Komesha ukimya –** usibaki mpweke: Pata msaada kutoka kwa mtu unayemwamini, au unaweza kuwasiliana na moja ya mashirika yanayotoa taarifa maalum na usaidizi

Kuna maisha baada ya kutoka kwenye uhusiano wa kinyanyasaji: Watu wengi hugundua kuwa wanafurahia kuishi bila patna na wengine huanzisha uhusiano mpya na wa mapenzi ambao hawakutegemea ungewezekana walipokuwa na patna wao mkatili.

2 Mpango wa usalama

Kufanya mpango wa usalama kutakusaidia wewe kujisikia una madaraka i zaidi na kukupa ujasiri wa kuchukua hatua za kujilinda wewe mwenyewe na watoto wako.

Hapa kuna vidokezi kadhaa vya kukusaidia kutayarisha mpango wa vitendo kwa ajili ya usalama wako

- Weka kitabu cha kumbukumbu ya matukio ya ukatili wa majumbani
- Fahamu ni wapi utaweza kupata simu kwa haraka na urahisi (ya mkononi, jirani, ndugu au rafiki)
- Jiwekee orodha ya namba za mawasiliano ya dharura, pamoja na ndugu, marafiki, polisi wa jirani
- Weka pesa kidogo kwa ajili ya basi wakati wa dharura
- Uwe na seti ya ziada ya funguo za nyumba
- Tunza funguo

Kama unapanga kuondoka, jaribu ku:

- Ondoka wakati una hakika mkosaji hayupo karibu
- Wachukue watoto wako wote
- Chukua karatasi za kisheria na kifedha, vyeti vya ndoa na kuzaliwa, amri za mahakama, kadi za NHS, pasipoti, liseni ya kuendeshea gari, vitabu vya ruzuku ya kodi ya watoto, kitabu cha anwani, vitabu vya benki, vitabu vya cheki, kadi za kukopea nk
- Chukua vitu binafsi vichache vyenye thamani itokanayo na hisia za moyoni
- Chukua vitu vya kuchezea watoto wavipendavyo sana
- Chukua nguo za kutosha siku kadhaa
- Chukua dawa zozote ambazo wewe au watoto wako huenda mkahitaji.

3 Kutoa taarifa polisi

Polisi wanalichukulia swala la ukatili majumbani kwa uzito mkubwa na watatoa kipaumbele kwa usalama wako

Kuna makosa kadhaa ambayo mtuhumiwa wa ukatili wa majumbani anaweza kushtakiwa nayo.

Katika dharura siku zote piga 999 kuomba msaada.

Kwa wakati mwingine unaweza kuzungumza na maafisa waliopewa mafunzo maalum kwenye:

Kitengo cha usalama wa jamii kwenye 020 7421 0326

Ni haki yako kutoa ripoti ya ukatili kwa polisi na kufanya hivyo kunaweza kukulinda wewe na watoto wako

Kama mtuhumiwa ameshtakiwa kwa kosa unaweza kulazimika kufika mahakamani. Kuna mashirika Islington ambayo yanaweza kukupa usaidizi ikiwa una wasiwasi juu ya kufika mahakamani. Wasiliana na moja ya mashirika yaliyopo kwa mbele ya kijitabu hiki kwa taarifa zaidi

4 Uchaguzi wa nyumba

Sheria ya nyumba inatambua kuwa ukatili majumbani unaweza kutokea katika mahusiano baina ya mapatna na baina ya wazazi na watoto wakubwa, vivyo hivyo na katika hali zingine.

Baadhi ya uchaguzi ulio nao ni:

Kubaki nyumbani au kurudi nyumbani ukiwa na ulinzi

Ulinzi wa kisheria – Unaweza kuiomba mahakama imwondoe mkosaji kutoka nyumbani, au kumkataza asikuingilie. Kwa taarifa zaidi kuhusu sheria, *angalia kifungu 5 – Fidia za kisheria*

Msaada kutoka mwenyenyumba wako – Kama unaishi kwenye nyumba ya halmashauri au ushirika wa wenye nyumba, mwenyenyumba wako anaweza kukusaidia ukaishi kwa usalama kwenye nyumba yako. Wasiliana na Ofisi ya Nyumba ya eneo lako au afisa wako wa nyumba kwa maelezo zaidi.

Kimbilio Nyumbani (Home Shelter) – Mpango huu unakupa hiari ya kubaki nyumbani kwako lakini kukiwa na hatua zaidi za kiusalama kama vile makufuli au visanduku vya barua visivyoweza kushika moto. Ili kustahili ni lazima uwe umefanyiwa vitendo vya kikatili hivi karibuni na ni lazima Halmashauri ya Islington waamini kuwa utakuwa ni mtu asiye na makazi kama utalazimika kuondoka nyumbani kwako kwa sababu ya nyumba yako kutokuwa salama. Ni lazima uwe mpangaji, mwenye hati ya kukodisha au mwenyenyumba. Wasiliana na:Kituo cha Misaada ya Nyumba cha Islington kwenye 020 7527 2000 kwa taarifa zaidi

Kwenda kwenye kimbilio la wanawake

Makimbilio ni nyumba zenye usalama zitoazo makazi ya muda kwa wanawake na watoto wanao toroka kutoka kwenye ukatili majumbani. Makimbilio mengi hupokea watoto wakiume hadi wenye umri wa 12 au 14. Anwani za makimbilio zinawekwa siri ili kuwalinda wanawake wanaokaa pale.

Wasiliana Masaa 24 Simu ya Kitaifa ya msaada Ukatili majumbani: Simu ya bure 0808 2000 247

Kudai kutokuwa na makazi

Halmashauri inao wajibu kisheria wa kukutafutia makazi ya muda wakati wakifanya utathmini. Sheria ya nyumba inasema: ‘Sio sawasawa kwa mtu kuendelea kukaa kwenye nyumba kama kuna uwezekano kuwa hii inaweza kuishia kwenye ukatili majumbani au ukatili mwingine’ Ukatili unamaanisha ukatili au vitisho vya ukatili kutoka kwa mtu mwingine, ambao kuna uwezekano kufanyika.

Wasiliana:
Kituo cha Misaada ya Nyumba cha slington ,
38 Devonia Road, London N1 8UY
Simu: 020 7527 2000

Kukaa kwa muda na rafiki au ndugu

Kama huu ni uchaguzi mzuri kwa kiasi utategemea

- Kiwango cha usaidizi wa kihisia na kimatendo ambao rafiki au ndugu anaweza kutoa
- Kama familia watakushawishi kuuendeleza uhusiano na kuufanikisha
- Kama patna wako/mkosaji anazijua anwani hizi na uwezekano wa kukufuata, kukutishia au kukushambulia wewe au watu unaokaa nao.

Upangaji binafsi au kununua nyumba

Kama ukiamua kupanga nyumba binafsi, unaweza kustahili msaada wa kulipia nyumba. Kituo cha Islington cha Misaada ya nyumba wanaweza kutoa ushauri kuhusu mikataba ya upangaji na taarifa kuhusu sehamu za kwenda kujaribu.

Lakini, mchakato wa kutafuta makazi mapya unaweza kuchukua muda mrefu, hivyo kwa sasa inaweza kuwa lazima kufanya mipango ya muda ya namna ya kuishi .

5 Fidia za kisheria

Kwenda mahakamani kunaweza kuonekana kunatisha lakini unatakiwa kukumbuka kuwa una haki ya kuishi bila woga wa ukatili. Mahakama inaweza kulinda haki zako.

Amri za kisheria za kukataza

Amri za kukataza zinapatikana kwenye sehemu ya IV ya Sheria ya Familia na zina madhumuni ya kukuweka salama. Utahitaji kumtafuta wakili wakukusaidia kujitayarisha kwa mahakama (wasiliana na moja ya mawakala wa usaidizi walio orodheshwa nyuma kwa taarifa kuhusu mawakili wa karibu) au utahitaji kutayarisha maombi yako mwenyewe (angalia amri za kukataza za kujitayarishia mwenyewe kwenye ukurasa unaofuata). Kuna amri za kukataza kuu mbili zinazoweza kukulinda. Hizi ni:

Amri ya kutosumbuliwa:
Amri hii inalenga kumzuia mkosaji asitumie au kutishia kutumia ukatili dhidi yako au mtoto wako, au kukuogofya, kukubugudhi au kukusumbua. Pia inaweza kuwazuia wasiweze kufikia umbali fulani kutoka kwenye nyumba yako. Madhumumuni ya amri ni kulinda afya, usalama na ustawi wa mwathiriwa na watoto wowote

Amri ya utwaaji:
Amri hii inaweza kumzuia mkosaji kuingia kwenye nyumba, hata kama kuna mkataba wa upangaji wa pamoja. Inaweza pia kumzuia mkosaji asifike kwenye maeneo fulani kwa mfano yadi 200 kutoka kwenye nyumba yako au shule ya mtoto.

Amri hizi zinaweza kuambatana na ‘uwezo wa kutia mbaroni’. Hii ina maana kuwa mkosaji akivunja masharti ya amri kwa namna yeyote, anaweza kukamatwa na hata kufungwa jela

Inawezekana kupata amri za kukataza ‘bila notisi’ Hii ina maana kuwa sio lazima mkosaji kuambiwa kuhusu mashauri mahakamani mapema. Hizi mara nyingi hutumiwa wakati wa dharura.

Mara nyingine mkosaji anaweza kutoa ‘ahadi’ kuwa hatakushambulia. Ahadi inatoa ulinzi mdogo kuliko amri ya kukataza na hulazimiki kuikubali.

Amri za kukataza za kuomba mwenyewe
Kama huna uwezo wa kumlipa wakili kwa sababu hustahili kulipiwa gharama za kisheria , unaweza kupeleka maombi ya amri ya kukataza wewe mwenyewe. Ili kukusaidia uweze kufanya hivi, Haki za Wanawake wametayarisha kiongozi kinachoelezea namna ya kujaza fomu ya maombi na kuomba moja kwa moja mahakamani.

Wasiliana na Haki za Wanawake kwenye:
020 7251 6577

Sheria ya kinga kutokana na bughudha ya 1997

Sheria hii ina manufaa hasa ikiwa unanyemelewa au kubugudhiwa na patna wako wa sasa au wa zamani. Utahitaji kumwambia wakili wako au mshauri wako wa kisheria kuhusu matatizo yanayokukabili na watakusaidia kuamua ni njia ipi nzuri ya kufuata.

6 Fedha

Wengi wa walio salimika wanakuwa na wasiwasi kuhusu hatari zinazo ambatana na kumalizika na uhusiano wa kinyumba, hasa kama walikuwa wanamtegemea kifedha patna wao. Usiruhusu hili kukuzuia kuomba msaada. Kama hufanyi kazi au unakipato kidogo, kuna ruzuku ambazo unaweza kustahili kuomba, pamoja na:

- Usaidizi wa kipato
- Ruzuku ya mtoto
- Ruzuku ya kodi ya nyumba
- Mkopo wa dharura
- Msaada wa ustawi wa jamii
- Nafuu ya kodi ya mtoto
- Watafutao kazi
- Ruzuku ya Kodi ya Halmashauri
- Mikopo ya Makisio

Kwa taarifa zaidi kuhusu ruzuku wasiliana na :

Ofisi ya Ushauri kwa Raia kwenye
www.citizensadvice.org.uk

Au angalia tovuti ya Idara ya Kazi na Pensheni kwenye

www.dfwp.gov.uk.

7. Watoto

Ni muhimu kukumbuka kuwa watoto wanadhurika kwa kushuhudia ukatili majumbani na watahitaji usaidizi ili waweze kuhimili yanayotokea nyumbani.Mara nyingine na watoto nao huwa wameumia au kutendewa vibaya.Kuna mashirika Islington ambayo yanaweza kukusaidia kuwalinda watoto wako kutokana na athari za ukatili majumbani.

Kwa taarifa kuhusu huduma za watoto Islington wasiliana na moja ya mashirika yaliyoorodheshwa nyuma ya kipeperushi hiki au nenda:

www.islington.gov.uk/childrensdirectory

Watenda mabaya kwa kawaida hutishia kuwa watoto wako watachukuliwa ikiwa utamwambia mtu yeyote kuhusu ukatili wa majumbani. Hii haina uwezekano wa kutokea hata kidogo. Huduma kwa Watoto wanatambua kuwa njia bora ya kuwalinda watoto wasidhurike ni kutoa usaidizi kwa mzazi au mtunzaji ambaye sio mtenda mabaya kwa manufaa ya watoto.

Kama una mashaka kuhusu ustawi wa watoto wako unaweza kuwasiliana na:

Huduma za watoto Islington Timu ya Utathmini kwenye 020 7527 7400

Au fika ofisini-

292 Essex Road, London, N1 3AZ.

Kama unafikiria kuondoka kwenye uhusiano wenye kutendewa vibaya jaribu kuondoka na watoto wako *(angalia Sehemu 2- Mipango ya usalama)*.

Kama umekwisha ondoka na una wasiwasi kuwa patna wako atawateka nyara watoto, kuna hatua ambazo unaweza kuchukua. Siku zote hifadhi hati za watoto wako (k.m. cheti cha kuzaliwa, pasipoti n.k.) na amri za mahakama zozote mahali penye usalama. Kama mtoto wako hana pasipoti, wasiliana na Ofisi ya Pasipoti na kuandikisha kukataa kwako kwa mtoto kupelekwa ng'ambo bila kibali chako. Ushauri zaidi kuhusu hili unaweza kupatikana kutoka kwa wakili wako, mshauri wa kisheria au Misaada kwa Wanawake.

Unaweza kuwa una wasiwasi kuhusu mawasiliano na mtoto baada ya kuachana na patna wako mkatili. Kama patna wako atataka kuwasiliana na mtoto , huna budi kuomba ushauri wa kisheria mapema iwezekanavyo.

Mahakama ni lazima wachukulie maanani athari za ukatili majumbani wakati wanashughulikia kesi zinazohusu mawasiliano na watoto. Hii itaweza kusaidia kuzuia walio salimika na watoto walio husika kwenye mabishano kuhusu mawasiliano wasiweze kufanyiwa ukatili zaidi.

Kuna masuala mbalimbali na amri za mahakama ambavyo vinalindwa na sheria:

- **Wajibu wa Wazazi –** mama wazazi moja kwa moja wanao huu. Baba wazazi walio waoa mama hawa wanao huu na baba aliyetajwa kwenye cheti cha kuzaliwa mtoto baada ya 2003 naye anao wajibu unaolingana na wa mama
- **Amri za Makazi –** hizi zinataja ni nani atakayeishi na mtoto
- **Amri za mawasiliano –** hizi zinahusu mawasiliano kati ya mzazi ambaye hakai nyumbani na watu wengine muhimu (k.m.wazazi wa wazazi na umbu), na mtoto. Mama anaweza kuiomba mahakama kuhakikisha kuwa mawasiliano yoyote yatakayo amriwa yawe chini ya usimamizi.
- **Amri za Mawasiliano chini ya Usimamizi –** kama hapo juu, hizi zinaagiza kuwa mawasiliano yoyote ni lazima yawe chini ya usimamizi.
- **Amri za Hatua Zilizokatazwa –** Ambazo zinawakataza wale waliotajwa kwenye amri wasifanye vitu fulani na mtoto, kama vile kumpeleka ng'ambo au kuwa na mawasiliano na mtoto yasiyo na usimamizi.

8 Masuala ya kuwa aina mbambali

Ukatili majumbani hutokea kwa watu wenye asili za aina zote

Mawakala walioorodheshwa nyuma ya kipeperushi hiki wanaweza kutoa usaidizi kwa watu wote bila kujali kabila, jinsia, umri au ulemavu. Lakini pia kuna mashirika mengi London na kokote Uingereza yanayoweza kutoa usaidizi kwa vikundi maalum

Orodha ya huduma hizi inapatikana kwenye:

www.islington.gov.uk/domesticviolence

Au unaweza kupiga simu mojawapo zilizopo kwenye jalada la mbele kwa taarifa zaidi.

Kama wewe unatoka kwenye **Jamii ya Weusi au Kabila dogo** unaweza ukapendelea kuwasiliana na shirika linaloshughulikia masuala maalum au linaloweza kutoa huduma katika lugha yako ya kwanza. Kwa nyongeza unaweza ukawa na wasiwasi kuhusu hali yako ya uhamiaji na jinsi inavyoweza kuathirika ukiondoka kutoka uhusiano wa kikatili. Unapaswa siku zote kuomba ushauri wa kisheria kuhusu **hali yako ya uhamiaji** na haki zako kabla hujafanya maamuzi. Kama unahofu kuwa huenda **ukaozeshwa kwa nguvu** kuna mashirika ya kiserikali na yakujitolea ambayo yanaweza kukusaidia.

Umri wako unaweza kuchangia katika kuamua ni shirika gani unajiamini zaidi kuwasiliana nalo. Tena kuna huduma zipatikanazo maalumu kwa **wanawake wenye umri mkubwa au mdogo**

Kuna baadhi ya huduma maalumu zipatikanazo kwa watu wenye vilema **vya kimwili** au **matatizo ya kujifunza** ambao wanafanyiwa ukatili majumbani.

Wasagaji na wanawake wenye jinsi mbili wanaweza kupata huduma sawa na zile zinazotolewa kwa wanawake wenye jinsi tofauti kwa kupitia Misaada kwa Wanawake na mashirika mengine ya kujitolea. Kama utapendelea kuwasiliana na shirika linaloshughulikia maalumu **wasagaji, wasenge, wenye jinsi mbili na waliobadilisha jinsi** wasiliana na Broken Rainbow.

Wanaume waliosalimika kutokana na ukatili majumbani wanaweza kuwasiliana na usaidizi wa waathiriwa wa Islington kwa msaada na taarifa. Unaweza pia kupiga simu ya misaada kwa wanaume, huku Broken Rainbow wakitoa misaada kwa wasenge na wanaume wenye jinsi mbili.

> ‘Mwisho wa yote mume wangu alifanya uchaguzi wa kuniumiza, Mimi sikushika mkono wake na kuupandisha usoni kwangu, yeye alifanya hivyo. Wakosaji hufanya uchaguzi.’

Kutoka misaada kwa wanawake ‘Wanawakewanazungumza’